# MWANASHERIA

JARIDA LA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS



TOLEO LA 002 JULAI - DISEMBA 2024

# "HAKI NA WAJIBU"

SCAN ME

Scan kusoma Jarida kielektroniki
www.agcz.go.tz

HALIUZWI

# SALAMU ZA MHE. MWANASHERIA MKUU



**KATIKA kuendelea na utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kuzitaka taasisi za umma kueleza shughuli zao na mafanikio ya utekelezaji wa shughuli hizo, Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, imeendelea na kazi ya kuandaa na kutoa JARIDA LA MWANASHERIA, kwa ajili ya kufanikisha utoaji wa elimu kwa umma. Elimu ya kuielewa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kuelewa shughuli za Afisi na masuala ya sheria kwa ujumla.**

Mbali na utekelezaji wa agizo la Serikali, utoaji wa elimu kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ni wajibu wa kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 14(1)(o) cha Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013.

Hivyo, uendelezaji utoaji wa Jarida hili ni utekelezaji wa sheria hiyo, jambo ambalo linaonesha utayari wa taasisi yetu katika utelekelezaji wa sheria za nchi, pamoja na utekelezaji wa majukumu ya msingi ya kikatiba ya Mwanasheria Mkuu, ambayo yanabainsha katika kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 (Toleo la 2020).

Katika toleo hili, tumeandaa Makala mbili muhimu kwa ustawi wa sekta ya sheria na ustawi wa jamii yetu. Makala moja inahusu Maadili. Makala hii inawakumbusha Maafisa wa Mahkama na Mawakili kutumikia majukumu yao kwa kuzingatia Maadili ya taaluma zao ili kujenga imani kwa jamii katika utekelezaji wa haki.

Kufuata maadili katika kazi ni muhimu kwa sababu kunamfanya mtumishi kuelewa anachohitajika na asichohitajika kukifanya katika utekelezaji wa majukumu ya kazi. **www.financierworldwide.com**, wanasema Maadili katika sehemu ya kazi yanamjenga mfanyakazi kwenye uaminifu na uadilifu, kuzingatia matakwa ya taaluma katika utendaji, kuwa ni mtu anayeweza kutegemewa, kukua kikazi na kuwa mtii wa sheria.

Kwa maana nyengine, maadili ni dira na muongozo wa utendaji kazi, ambao hatimae unajenga heshima ya watendaji kazi na kuchangia ufanisi wa kazi.

Madhumuni ya Makala hii ni kuwafanya watumishi wetu katika Sekta ya Sheria kwa ujumla, na kipekee kwa Sekta ya Utoaji wa Haki, kuyazingatia hayo na kuyatekeleza ili Sekta ya Sheria na muhimili wa utoaji wa haki uweze kuaminika mbele ya macho ya umma na iwe ni sehemu ya kukimbilia kwa wanaotafuta haki, badala ya kuwa ni sehemu inayotisha na kukimbiwa.

Makala nyengine katika Toleo hili inahusu Utaratibu wa Kufungua Madai dhidi ya Serikali. Utaratibu huo upo kwa mujibu wa Sheria ya Madai ya Serikali *Nam. 3 ya 2010 (Government Proceedings Act 2010).* Makala hii inaeleza hatua za kufuatwa kwa mtu anayetaka kufungua mashauri ya madai dhidi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ni jambo la wazi kwamba katika miaka ya karibuni, kutokana na kukua kwa harakati za kiuchumi, harakati za kisiasa, na maingiliano makubwa katika shughuli za kijamii, pamoja na kuongezeka kwa uwazi katika masuala ya haki na sheria, umekuwepo mwamko mkubwa wa watu kutaka kudai haki zao. Katika hali hiyo, Serikali inahusika kudaiwa baadhi ya haki hizo.

Kwa utaratibu uliowekwa na sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa naiba ya Serikali ndio inayosimamia kesi za madai ambazo Serikali inashtakiwa au inashtaki.

Kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Mashauri ya Madai ya Serikali kinaeleza kuwa kesi yoyote ya madai baina ya Mdai na Serikali itafunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu.

Kwa matakwa hayo ya kisheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio inayohusika na kesi za aina hiyo. Kwa hivyo, Afisi inaelewa kwa kina hali ya utekelezaji wa jukumu hilo pamoja na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake.

Miongoni mwa changamoto hizo ni kukosewa kwa utaratibu wa kufungua mashauri hayo, na hivyo kuchelewesha mchakato wa kufungua mashauri ya aina hiyo.

Tumeona ni vizuri kuweka mada hii, katika Toleo hili la Jarida la MWANASHERIA. Lengo likiwa ni kusadia taasisi za umma pamoja na jamii kuelewa kwa kina zaidi hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kufungua mashtaka dhidi ya Serikali, ili kupunguza changamoto zinazojitokeza wakati wa kufunguliwa kwa mashtaka ya aina hiyo na kuharakisha mchakato wa kufunguliwa hadi kusikilizwa mashtaka hayo.

Tunatumai wasomaji wa Jarida letu watapata faida inayotarajiwa. Hivyo, tunawaalika kulisoma Toleo hili ili waweze kufaidika na Makala zake pamoja na habari mbali mbali zilizomo.

Kwa kufanya hivyo, watajiongezea upeo katika kuelewa shughuli tunazotekeleza katika Afisi yetu, na shughuli zinazotekelezwa katika Sekta ya Sheria kwa ujumla.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uwezo wa kulikamisha Toleo hili. Vile vile, napenda kuwashukuru watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa mchango wao katika maandalizi ya Toleo hili, hasa wale waliohusika moja kwa moja na matayarisho yake.

Aidha, tunatoa shukrani maalum kwa waandaaji wa Makala na taarifa mbali mbali za Toleo hili. Pamoja na hao, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa wasomaji wetu wote wa Toleo la Kwanza la Jarida hili.

Baadhi ya wasomaji hao wametueleza furaha yao kwa ujio wa Jarida hili na miongoni mwao wametuletea maoni mbali mbali, kwa lengo la kuliimarisha zaidi ili kufikia kiwango cha juu zaidi cha ubora.

Sisi katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, tumeyapokea maoni yao na tumeyafanyia kazi kwa lengo la kutoa matoleo yaliyo na ubora zaidi hapo baadae.

Zaidi, tunawakaribisha wasomaji waliobahatika kusoma Toleo la Kwanza la Jarida letu, wajipe muda kwa ajili ya kujisomea Toleo hili jipya. Aidha tunawaomba wasomaji wetu kutoa maoni yao kupitia anuani na mawasiliano hapo chini na tunaahidi kuyafanyia kazi.

**Dkt. Mwinyi Talib Haji,**
**Mwanasheria Mkuu,**
**Zanzibar.**

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

**Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar**

**S.L.P 259**
**Mazizini, Zanzibar, Tanzania.**
**Simu : + 255 22 233455**
**barua pepe: agcsmz@agcz.go.tz**
**www.agcz.go.tz**

SCAN ME




**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
Shaaban Ramadhan Abdalla
(Naibu Mwanasheria Mkuu)

**Wajumbe**
Mdungi M. Mdungi
Salim M. Abdalla
Asya M. Ahmed
Shufaa A. Khamis
Abeid M. Saleh
Hamisa Mmanga
Faki H. Mjaka

**Msanifu**
Abdulghani I. Zubeir

**Mshauri**
Ramadhan M. Suleiman


# TAHARIRI

**KWA dhati kabisa tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uwezo wa kukamilisha Tolei hili la Pili la Jarida la MWANASHERIA ambalo sasa lipo tayari kwa matumizi ya wadau.**

Toleo hili limekamilishwa kwa Makala mbili, habari zinazotokana na shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, shairi moja na kibonzo. Aidha, picha mbali mbali zimetumika kupamba Makala na habari za Jarida.

Makala moja ya toleo hili inahusu Maadili kwa Maafisa wa Mahkama na Mawakili na Makala nyengine inaeleza Utaratibu wa Kufungua Mashauri ya Madai dhidi ya Serikali.

Makala hizi zinajipambanua na zinatofautiana kimalengo na kimaudhui.

Makala ya Maadili inazungumzia haja iliyopo kwa Maafisa wa Mahkama kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya maadili ya taaluma zao, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa haki na ufanisi.

Makala nyengine inaeleza hatua za kufuatwa katika kufungua Mashauri ya Madai dhidi ya Serikali, ili kutoa elimu kwa umma juu ya hatua hizo, na iwe rahisi kuzifuata ikitokea haja.

Kuhusu habari, Toleo hili linajumuisha mada tofauti ikiwemo maelezo ya kumuaga aliyekuwa mtumishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Bi Mtumwa Said Sandali (Mwanasheria wa Serikali) ambaye alipata uteuzi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini ZMA; Taarifa ya Ziara ya Kuwaelimisha Wananchi wa Shehia ya Mzuri Makunduchi, Shehia ya Bambi na Shehia ya Nungwi Kiungani kwa upande wa Unguja. Kwa pande wa Pemba Shehia ya Stahabu pamoja na Shehia ya Tumbe Mashariki kuhusu masuala ya Sheria, ambayo ni sehemu ya Programu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu ya kuwafikia wananchi (Outreach).

Taarifa nyengine inahusu Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) baina ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Sheria, Jodhpur, India (NLUJ) na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar; na Taarifa kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kuunganishwa tena na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, katika utekelezaji wa agizo la Serikali la kuziweka pamoja taasisi hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mchanganyiko huo wa makala na taarifa mbali mbali, pamoja na picha unalifanya Toleo hili kutimiza miongoni mwa malengo ya Afisi yetu ya kuuarifu umma juu ya shughuli tunazofanya katika Afisi yetu na kutoa elimu na baadhi ya mafunzo yanayohitajika, kupitia Jarida hili.

Kukamilika kwa Toleo hili ni matunda ya kazi nzuri iliyotekelezwa kwa ushirikiano mkubwa baina ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu chini ya usimamizi wa Mhe. Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu, Wajumbe wa Bodi ya Wahariri, Waandalizi wa Makala (Wataalamu), Idara zote za Afisi ya Mwanasheria Mkuu chini ya Wakurugenzi.

Wengine ni Wanasheria wa Serikali katika Idara hizo, maofisa pamoja na watumishi wengine wa Idara hizo, ambao kila mtu kwa nafasi yake na kwa ujumla wao wana mchango mkubwa katika kufanikisha maandalizi ya Toleo hili.

Kwa dhati kabisa, kwa niaba ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar tunatoa shukrani kwa mchango wao katika kufanikisha kukamilika kwa Toleo hili. Vile vile, tunawashukuru wachapishaji wa Toleo hili kwa kazi nzuri ya kulitoa Jarida hili katika hali nzuri kama linavyoonekana.

Aidha, tunawashukuru watu wote ambao kwa namna moja au nyengine wameshiriki kufanikisha kazi hii ambao hawakutajwa hapa, kwa ushiriki wao ambao bila shaka una mchango mkubwa katika kukamilika kwa kazi hii.

Kwa hao wote tunasema tunauthamini mchango wao na tunakaribisha ushiriki wao katika matoleo mengine yatakayofuata. Mwisho, tunatoa shukrani za awali kwa wasomaji wa Toleo hili na tunakaribisha maoni yao kwa anwani za mawasiliano zifuatazo:

**Afisi ya Mwanasheria Mkuu**
**Zanzibar,**
**SLP 259,**
**Mazizini, Zanzibar, Tanzania**
**Simu: +255 22 233455**
**Barua pepe: agcsmz@agcz.go.tz**
**Tovuti: www.agc.go.tz**

**Shaaban Ramadhan Abdalla**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri**



*Wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Taasisi nyengine za SMZ waliohudhuria mafunzo maalum ikiwemo Mikataba, wakiwa katika picha ya pamoja na Uongozi wa Chuo Kikuu cha NLUJ nchini India.*

# AFISI ya Mwanasheria Mkuu, NLUJ wasaini MoU

**NA MWANDISHI WETU**

AFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Sheria Jodhpur cha India (NLUJ), zimesaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano (MoU) katika kujengeana uwezo kwenye sekta ya sheria.

Makubaliano hayo yamesaniwa na Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban R. Abdalla na Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Sheria Jodhpur cha India (NLUJ), Profesa Harpreet Kaur, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo hicho kilichopo jimbo la Jodhpur nchini India.

Akizungumza mara baada ya kusaini hati hiyo, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, alisema makubaliano hayo yatatoa fursa kwa watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Wanasheria wengine wa SMZ, kuongeza maarifa na utaalam katika maeneo mbali mbali ya fani ya Sheria.

Alibainisha kuwa NLUJ, ni chuo chenye historia nchini India ambacho kimeleta mapinduzi katika uwanja wa taaluma ya sheria, hivyo watendaji watapata fursa kuongeza ujuzi kutokana na uzoefu wa wataalam wa sheria wa chuo hicho.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo cha NLUJ, Profesa Harpreet Kaur, alisema kuwa, makubaliano hayo sio tu yatakuza juhudi za kitaaluma kati ya Zanzibar na India, bali pia yatakuza urafiki na kubadilishana utamaduni wa nchi hizo.

Alifafanua kuwa, makubaliano hayo pia yatazingatia kubadilishana maarifa na tafiti mbali mbali za kitaaluma.

Aidha, kupitia makubaliano hayo, programu za mafunzo ya kujengeana uwezo zitaendeshwa ambazo zitakuwa zikifanywa kwa nadharia na vitendo huku zikiongozwa na matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Prof. Harpreet aliongeza kuwa, makubaliano pia yatatoa fursa kwa vitivo katika chuo hicho, wanafunzi, Mawakili wa Serikali, Maafisa sheria na Watafiti kutoka taasisi hizo mbili, kufanya tafiti kuhusu mada mbalimbali zinazohusiana na Sheria kama vile usuluhishi, mikataba, biashara, usimamizi wa kesi za madai, utatuzi mbadala wa migogoro na uandishi wa sheria kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Chuo cha NLUJ, Dk. Neeti Mathur, alisema ana matumaini kuwa kila upande utanufaika vyema na makubaliano hayo yanayohusu taaluma na kujengeana uwezo.



*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban R. Abdalla na Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Sheria Jodhpur cha India (NLUJ), Profesa Harpreet Kaur, wakisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika kujengeana uwezo kwenye sekta ya sheria katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Chuo hicho Jimbo la Jodhpur nchini India.*

Aidha Mkurugenzi Rasilimali Watu, Utawala na Mipango kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Fatma Idd Ally, alimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji kwa kuchukua juhudi binafsi za kuomba mafunzo maalum ya usimamizi wa mikataba na mapatano katika Mikataba kwenye ubalozi wa India kwa watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo yamekuwa na umuhimu mkubwa.

Vile vile Mkurugenzi Fatma aliahidi kuwa watayatumia vyema mafunzo waliyopatiwa, ili kuongeza tija na kasi ya utendaji kazi zao kwa faida ya Serikali na Taifa kwa ujumla.

Mafunzo hayo ya wiki mbili ya Mawakili na Maafisa Sheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar pamoja na Wanasheria wa SMZ, yalifanyika Jodhpur nchini India.



*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban R. Abdalla kushoto na Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Sheria Jodhpur cha India (NLUJ), Profesa Harpreet Kaur, wakionesha Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) mara baada ya kuzisaini katika Chuo hicho huko Jimbo la Jodhpur nchini India.*

# Yafahamu maadili ya taaluma ya Sheria




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar ambapo mara nyingi husisitiza umuhimu wa kufuata maadili kwa Wanasheria.*

**MAADILI ni nguzo muhimu katika taaluma zote ikiwemo sheria. Ukosefu wa maadili ni chimbuko la utovu wa nidhamu na mithili ya jahazi iliyokosa mwelekeo.**

Taaluma ya sheria inayojumuisha Maafisa wa Mahkama, Mawakili wa Serikali na binafsi, Wanasheria na taasisi nyengine za sheria, kwa kipindi hiki zimebahatika kupata idadi kubwa ya wataalamu wapya wenye umri mdogo.

Ni busara kukumbushana uimarishaji wa maadili. Dhana ya maadili ni kubwa lakini makala hii inakusudia kueleza dhana ya maadili kwa upande wa Mahkama na Mawakili ili kujenga imani ya haki kutendeka na kuonekana kutendeka.

**Maana ya Maadili ya Sheria**

Wanafalsafa mashuhuri mbali mbali akiwemo Professa Kraus, Plato, Robert Burns, Benjamin Cardozo, Socrates na Aristotle wameeleza maana ya maadili ya sheria. Ufupisho wa tafsiri ya maadili kwa mujibu wa wanafalsafa waliotajwa hapa ni: mkusanyiko wa tabia, taratibu na msingi maalum ambayo mwanataaluma analazimika kuiamini na kuiheshimu ndani na nje ya utekelezaji wa kazi zake.

**Madhumuni ya Maadili**

Madhumuni makubwa ya maadili ni kujenga imani kwa jamii ya kutekeleza haki bila ya kuipindisha. Sababu hii inaungwa mkono na msemo wa kilatini unaosema "haki itendeke hata mbingu zikianguka". Maana ya msemo huu ni haki itendeke bila ya kujali athari zitakazotokea.

Aidha, kauli ya marehemu Mwalimu Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kazi ya kuhukumu kwa kutoa haki haifanywi na kila mtu. Hii ni kazi maalum kwa watu wenye maadili yasiyotiliwa shaka.

**Maadili kwa upande wa Mahkama**

Kigezo kikubwa cha misingi mikubwa ya maadili kwa upande wa Mahkama ni Misingi ya Bangalore "Bangalore Principles" iliyopitishwa katika kikao cha Majaji Wakuu kilichofanyika India, mwaka 2001. Misingi mikuu ya maadili kwa maafisa wa Mahkama ni hii ifuatayo:

**Uhuru na maamuzi:** Afisa wa Mahkama atekeleze kazi zake kwa uhuru na maamuzi anayofikia ni kwa mujibu wa tathmini ya taarifa alizopata na ufahamu wake wa sheria bila ya kubabaishwa na mashinikizo au ushawishi kutoka sehemu yoyote.

Msingi huu umeungwa mkono




*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji (katikati) akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa kongamano la mwaka la Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria lililofanyika ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA Maruhubi, Zanzibar.*

na kesi mbali mbali zilizoamuliwa ndani na nje ya nchi. Kwa mfano, kesi ya *Locabail (UK) Ltd v. Bayfield Properties Ltd [2000] QB 451* ambayo kimsingi inaeleza mazingira ya Jaji kujiondoa katika kusikiliza kesi ikiwa kuna mazingira ya upendeleo au mgongano wa maslahi au kutoweza kutekeleza haki (recusal).

**Uadilifu:** Afisa wa Mahkama atekeleze kazi bila ya upendeleo au kupangiwa kabla ya kesi na kuleta madhara upande mwengine. Vile vile, Afisa wa Mahkama awe na tabia ya kuheshimika ndani na nje ya Mahkama ili kujenga imani.

Kwa muktadha wa maelezo haya, Afisa wa Mahkama anapaswa kujiepusha kusikiliza kesi ambayo atakuwa na upendeleo au maslahi.

Aidha, Afisa wa Mahkama anatakiwa awe mtulivu, anajiheshimu, asikilize maelezo kwa makini, kuongea na wadaawa wa kesi, mashahidi, mawakili watu wengineo kwa busara. Msingi huu umeungwa mkono na mwanafalsafa Socrate.

Ni busara Afisa wa Mahkama akajiepusha kufanya vikao ndani ya ofisi yake na wadaawa wa upande mmoja na wakati huo huo wadaawa wa upande mwengine wa kesi wakawekwa nje. Jambo hili ni chanzo cha malalamiko.

**Kujiheshimu:** Kitendo cha Afisa wa Mahkama kujiheshimu kunajenga imani ya wananchi ya utendaji wa haki na kuonekana kutendeka.

Baadhi ya wataalamu wa sheria wamefanya uchambuzi na kutanua wigo wa neno kujiheshimu kutoka kwa Afisa wa Mahkama hadi kwa wanafamilia wa Afisa wa Mahkama.

Kitendo cha mwanafamilia ya Afisa wa Mahkama kinaathiri kwa njia moja au nyengine imani ya wananchi ya upatikanaji wa haki. Ni wajibu wa Afisa wa Mahkama kuchunga tabia na mwenendo wa wanafamilia wote na hata marafiki zake.

**Tabia na upole:** Afisa wa Mahkama ajichunge tabia kiujumla katika maisha yake ya kila siku na tabia ifanane na heshima ya nafasi aliyonayo na kamwe asitumie ofisi yake kwa maslahi binafsi.

Ni lazima aepuke mazingira ya kutiliwa shaka ya tabia na mwenendo wake. Ijapokuwa Afisa wa Mahkama anayo haki ya kikatiba ya kutoa maoni yake lakini achunge ulimi namna ya kutoa maoni yake kwa kuzingatia heshima ya ofisi yake. Vile vile, Afisa wa Mahkama awe makini wa kuchagua hata maeneo anayotembelea ili asitiliwe shaka.

**Usawa:** Afisa wa Mahkama atekeleze kazi kwa msingi wa usawa kwa watu wote bila ya kujali imani zao za dini, ukabila, asili ya mtu, jinsia, umri na hali ya uwezo wa mtu kiuchumi.

Asiwe na tabia ya ubaguzi wala upendeleo wowote kwa vitendo au maneno yake. Hali hii itajenga imani kwa jamii ya utendaji wa haki katika kazi zake.

Uweledi na uangalifu: Afisa wa Mahkama analazimika kuongeza ujuzi kwa kusoma maandiko mbali mbali ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa uweledi wa hali juu na kuendeleza sayansi ya sheria ya kufikiri na kufanya uchambuzi wa mambo.

Kwa msingi huu, Afisa wa Mahkama asiridhike na elimu na ujuzi aliokuwa nao. Awe mbunifu na anayefikiri zaidi ya uwezo wa kufikiri mtu wa kawaida. Hatua hii itaendeleza sayansi ya sheria (jurisprudence).

**Maadili kwa Upande wa Mawakili**

Kimsingi, maadili ya mawakili hayatofautiani sana na maadili ya Maafisa wa Mahkama. Kada mbili hizi zinatumikia taaluma moja ya sheria ijapokuwa wanatofautiana nyadhifa za kazi wanazofanya.

Katika kitabu chake, Lord Denning, '*(the Discipline of Law, Oxford University Press, 1, 1979)*', imesisitizwa kwamba wakili ni sawa na Jaji (Afisa wa Mahkama) anayo majukumu mbele ya Mahkama na kosa kufikiria kwamba wakili ni msemaji wa mteja wake kwa jambo lolote analolitaka. Ni wajibu wa wakili kuzingatia haki na ukweli wa maelezo ya mteja wake.

Maadili ya msingi ya mawakili katika utekelezaji wa majukumu ni

haya yafuatayo:

**Usiri:** Ni wajibu wa wakili kuhifadhi siri za mteja wake na haruhusiki kuzitoa siri hizo isipokuwa atakaporuhusiwa na mteja wake.

Hivi sasa, inasikitisha baadhi ya mawakili wanashindwa kuzuia vifua vyao na badala yake wanatoa siri za wateja wao jambo ambalo linadhalilisha taaluma ya sheria.

**Uadilifu:** Mithili ya Maafisa wa Mahkama, mawakili nao wanalazimika kuwa waadilifu katika utendaji wa kazi zao ili kunusuru heshima ya taaluma. Uadilifu ni pamoja na kujiepusha na vitendo vya ulaghai, udanganyifu, hila au hadaa. Inajumuisha na vitendo vya kuficha nyaraka ili kuzuia haki kutendeka.

**Uweledi:** Wakili analazimika kuongeza ujuzi kila siku kwa kusoma maandiko tofauti na maamuzi ya kesi za ndani na nje ya nchi. Haipendezi wakili kujilemaza kitaaluma na kila siku kutumia kesi hizo kwa hizo katika kujenga hoja dhidi ya upande wa pili.

Kinyume na miaka iliyopita ambapo upatikanaji wa maandiko ilikuwa unahitaji juhudi maalum. Kwa wakati uliopo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, taarifa za kimahkama na taaluma ya sheria zinapatikana katika mitandao.

Wajibu wa Wakili kwa Mahkama: Wakili ni Afisa wa Mahkama na awajibika kuiheshimu Mahkama. Aidha, wakili anatakiwa ajenge hoja kwa mujibu wa sheria badala ya kuegemea majungu.

Ni wajibu wa mawakili kujitathmini na kulinda wajibu wake akitambua kwamba Mahkama inafanya maamuzi kwa mujibu wa hoja za kisheria zinazotolewa na mawakili katika kesi.

Wajibu wa Wakili kwa Mawakili



*Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar Mhe. Ibrahim Mzee akiwa katika kongamano la mwaka la Mawakili na Maafisa Sheria wa Serikali lililoambatana na mafunzo ya kuwajengea uwezo lililofanyika katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA Maruhubi, Zanzibar.*

**Wenzake:** Wakili analazimika kuheshimu na kuvumilia hoja kinzani zinazotolewa na wakili wenzake. Mashirikiano ni lazima ikiwemo kubadilishana nyaraka ili kuhakikisha haki inatendeka.

**Mgongano wa Maslahi:** Wakili lazima aepuke mgongano wa maslahi. Tafsiri ya mgongano wa maslahi ni pana lakini kwa ufupi ni jambo lolote linallomhusu kwa mfumo wowote ambao utaathiri upatikanaji wa haki.

Kwa mfano, kesi inayomhusu rafiki au ndugu yake, amepata mkopo kutoka mtu au taasisi, kupokea zawadi au kushiriki binafsi au ndugu yake katika shauri na baadaye kutakiwa kulisimamia mahkamani.

Misingi iliyotajwa hapo juu ya Maofisa wa Mahkama na Mawakili ni baadhi ya misingi wanayotakiwa wanataaluma hawa kuiheshimu katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Tunaipongeza Mahkama, mwanzoni mwa mwaka 2024 imeunda Kamati ya Maadili kwa Mawakili. Aidha, Kamati ya Maadili kwa Majaji na Mahakimu inaundwa pale inapohitajika (ad-hoc committee).

Kimsingi, maadili ya Maafisa wa Mahkama na Mawakili yanafanana na "Bangalore Principles" ya mwaka 2001. Kesi za ukiukwaji wa maadili dhidi ya mawakili tayari zimefikishwa katika Kamati husika.

Watu wanaohisi misingi ya maadili kwa Maafisa wa Mahkama au mawakili imekiukwa ni vyema wakawasilisha malalamiko yao katika kamati husika badala ya kulalamika bila ya kupata tija.

**Makala hii imetayarishwa na Dk. Ali A. Uki Mkuu wa Skuli ya Sheria Zanzibar.**

# Watendaji Afisi ya Mwanasheria Mkuu wahimizwa kufuata maadili



*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban R. Abdalla akifungua mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA, Maruhubi mjini Zanzibar.*

**NA MWANDISHI WETU**

**AFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, imewasisitiza wafanyakazi wa taasisi hiyo kufuata maadili ya utumishi wa umma kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao ili kuleta faida kwa serikali na taifa kwa ujumla.**

Akifungua mafunzo kwa wafanyakazi wa Afisi hiyo huko katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA Maruhubi Mjini Unguja, Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban R. Abdalla, alisema endapo watendaji hao watatekeleza majukumu yao kwa kufuata misingi ya maadili watakuwa kimbilio la wananchi wanaohitaji huduma.

Naibu Mwanasheria Mkuu huyo, alibainisha kuwa Afisi imeandaa mafunzo hayo ambayo yatawasaidia kuwapatia elimu na kukumbusha juu ya umuhimu wa uadilifu kwenye utendaji hatua ambayo itaongeza ufanisi na kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Sisi kama viongozi ni wajibu wetu kuandaa mafunzo ya kuwakumbusha watendaji wetu majukumu yao, ili waendelee kuyatekeleza kwa ufanisi", alisema Naibu Mwanasheria Mkuu.

Akiwasilisha mada ya maadili ya Utumishi wa Umma, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Ndg. Omar Haji Gora, alieleza kuwa miongoni mwa maadili hayo ni kutunza siri za Afisi, kujali na kuzingatia wakati, utii kwa viongozi na kuvaa nguo za heshima.

Akielezea umuhimu wa kuzingatia maadili katika taasisi Ndg. Gora alisema, husaidia kukuza utamaduni wa uaminifu na uwajibikaji wa taasisi, hukuza heshima ya Taasisi, huongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma bora na huwavutia wateja.

Kwa upande wake, Mhandisi Suleiman Abdallah akiwasilisha mada kuhusu usimamizi wa mikataba, aliwataka wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na utaratibu wa kujiongezea maarifa hasa kuhusiana na maendeleo ya teknolojia ili kuifahamu mikataba

inayoletwa Afisini kwao kwa lengo la kuitolea ushauri wa kitaalam.

Kwa upande wa washiriki waliopatiwa mafunzo hayo, walisema wamejifunza mambo mengi ya msingi yatakayochochea kasi ya utekelezaji wa majukumu yao huku wakiahidi kwenda kuifanyia kazi elimu walioipata kwa vitendo.

Aidha, wafanyakazi hao waliuomba uongozi wa Afisi yao kuendelea kutoa mafunzo hayo ambayo ni muhimu katika kuwakumbusha majukumu yao pamoja na kupata mbinu mpya za kukabiliana na changamoto za kiutendaji pale zinapojitokeza.

Jumla ya mada tatu ziliwasilishwa katika mafunzo hayo ambazo ni Maadili na Uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma, Usimamizi wa Mikataba pamoja na Afya ya Akili ambapo washiriki wa mafunzo hayo pia walipata fursa ya kuzijadili.



***Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Ndugu Omar Haji Gora, akiwasilisha mada ya maadili ya Utumishi wa Umma kwa Wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA Maruhubi, Zanzibar.***



***Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Kesi za Madai kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Ndugu Ali Ali Hassan akichangia mada katika mafunzo ya ndani ya kuwajengea uwezo wafanyakazi yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha SUZA Maruhubi, Zanzibar.***



# Ufahamu utaratibu wa kufungua madai dhidi ya Serikali

**SERIKALI ni taasisi ambayo kwa kuwa inaongozwa na wanadamu inatokea kufanya makosa ya kimadai kama ilivyo kwa watu binafsi, hivyo mtendaji wa Serikali anapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yake akifanya kosa la kimadai muathirika wa matendo hayo anaweza kufungua kesi ya madai.**

Dhana ya kuifungulia madai Serikali sio mpya, bali ilikuwepo tangu wakati wa utawala wa kikoloni. Mnamo 1917 wakati Sheria ya Mwenendo wa Madai ya 1917 (Sura ya 8) ilipoidhinishwa na Watawala wa kikoloni kutumika hapa Zanzibar, ilikuwa na masharti ya kufungua madai dhidi ya Serikali.

Sehemu ya IV ya Sheria hiyo iliweka utaratibu wa kufungua madai mahakamani dhidi ya Serikali. Kifungu cha 59 cha Sheria hiyo kilieleza kwamba Serikali inapotaka kufungua madai dhidi ya mtu au taasisi yoyote mdai awe ni "British Resident" ambaye kwa sasa na kwa mujibu wa Sheria Kutafsiri Sheria na Masharti ya Jumla Nam. 7 ya 1984 ni Waziri husika.

Kifungu cha 60 cha Sheria hiyo kiliweka masharti ya kufungua madai dhidi ya Serikali ambayo ni; Mdai lazima awe ametoa notisi ya miezi miwili ya kutaka kuishtaki Serikali na muda huo uwe umetimia

Sharti jengine Notisi hiyo itumwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali; au Mkuu wa Wilaya ile ambapo tatizo limetokea; na Notisi ieleze sababu za madai, jina, maelezo binafsi na mahala anapoishi Mdai pamoja na shufaa anayoomba.

Sheria hii haikuweka mahkama maalum ambayo



*Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar (kushoto), Ndg. Shaaban R. Abdalla wakiwa katika Ukumbi wa Mahkama kufuatilia kesi ya Madai dhidi ya Serikali.*

madai yanayohusisha Serikali yangefunguliwa. Ndio maana Serikali iliweza kufunguliwa madai katika mahakama za chini kulingana na thamani ya kitu kinachodaiwa. Kifungu cha 59 na 60 vilifutwa na Sheria ya Madai ya Serikali *Nam. 3 ya 2010 (Government Proceedings Act 2010)*, na sasa utaratibu umebadilika kidogo.

**Sheria ya Madai ya Serikali *Nam. 3 ya 2010 (Government Proceedings Act 2010)***

Masharti kuhusu utaratibu wa kufungua madai dhidi ya Serikali yaliyokuwepo tokea 1917 yaliendelea kutumika hadi 2010 ilipotungwa Sheria ya Madai ya Serikali nam. 3 ya 2010 (Government Proceedings Act 2010).

Sheria hiyo ilikuja kurekebisha kidogo utaratibu wa kufungua madai dhidi ya Serikali kwa kueleza wazi kwamba Serikali itawajibika kwa dhima zote katika mikataba, madhara na katika mambo yote mengineyo ambayo mtu mwenye uwezo kisheria angeweza kuwajibika.

Hivyo, mtumishi wa Serikali anapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yake akifanya kosa lolote la kimadai, Serikali ndio inayopaswa kufunguliwa madai. Swali linaweza kuwa ni nani atakayefunguliwa madai hayo? Kifungu cha 10 cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba, bila kuathiri masharti mengine yoyote ya Sheria, Madai ya Serikali yatafunguliwa na Mwanasheria Mkuu (Mdai) na iwapo mtu anafungua madai dhidi ya Serikali madai hayo yatafunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu (Mdaiwa).

Kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Mwanasheria Mkuu ni Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na atatekeleza kazi nyengine za kisheria atakazopelekewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi au atakazopewa kwa mujibu wa Katiba au Sheria nyengine.

Aidha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam 6 ya 2013 pamoja na mambo mengine, inampa nguvu za kisheria Mwanasheria Mkuu kusimamia na kuendesha kesi zote za madai za Serikali kama kifungu za 16 cha Sheria Namba 6 ya 2013

kinavyobainisha.

Kwa mujibu wa muundo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Idara ya Usimamizi wa Kesi za Madai ndio iliyopewa kazi ya kutekeleza majukumu hayo kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu. Miongoni mwa kazi hizo ni kuiwakilisha serikali na taasisi nyengine za umma katika kesi za madai, usuluhishi na mienendo mingine ya madai.

Kitu cha msingi kufahamu ni kwamba si kila tendo la kimadai linalofanywa na mtumishi wa umma hushtakiwa Serikali, bali ni yale matendo yanayofanywa na mtu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikazi.

Kwa maneno machache tuseme kwamba hakuna sababu ya madai (cause of action) dhidi ya Serikali pale ambapo mtumishi amefanya tendo lolote dhidi ya mtu mwengine akiwa nje ya utekelezaji wa majukumu yake ya kazi.

**Utaratibu Mpya wa Kuifungulia Madai Serikali**

Kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Madai ya Serikali nam.3 ya 2010, utaratibu wa kufungua madai dhidi ya Serikali ni huu ufuatao:

Notisi ya maandishi ya kutaka kufungua madai dhidi ya Serikali. Notisi hii ni ya miezi miwili na itumwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Mwanasheria Mkuu. Neno "na" limewekwa kwa makusudi na sio "au" kama inavyofanywa na watu wengi wanapotuma notisi hii.

Aidha kumtolea nakla Mwanasheria Mkuu haijakidhi matakwa ya sheria. Ili notisi ikubalike kuwa notisi, ni lazima masharti yake yatimie kama inavyoelezwa na *kifungu cha 6(1) cha Sheria Nam. 3 ya 2010* kwa kueleza sababu ya madai, jina, maelezo na anapoishi mdai pamoja na shufaa anazolalamikia na hati ya madai yenye taarifa kwamba notisi imetolewa.

Hivyo kama kuna hati yoyote ambayo ingetumika kama kielelezo inabidi kuambatanishwa na notisi hiyo ili kutoa fursa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kushughulikia lalamiko hilo kikamilifu.

Mara notisi hiyo inapopokelewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu hufanyiwa kazi kwa kufanya mahojiano na taasisi inayolalamikiwa. Ikionekana kwamba madai ya Mdai ni ya msingi, Afisi ya Mwanasheria huishauri taasisi inayolalamikiwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza na hapo Mlalamikaji hupatiwa shufaa anayoomba bila kwenda mahakamani.

Kama muafaka haukufikiwa au kwamba maelezo yatakayopatikana kwa taasisi husika itaonekana kwamba mlalamikaji hana madai ya msingi, hujibiwa hivyo na ana hiari kusamehe au kufungua kesi ya madai mahakamani dhidi ya Serikali. nakla ya Hati ya Madai inatakiwa kupelekwa



***Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakiwa katika Afisi ndogo iliyopo Mahkama Kuu Tunguu, katika usikilizaji wa kesi za Madai dhidi ya Serikali.***

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mbarouk Mselem Shazil akitoa elimu ya kisheria kwa wananchi wa Nungwi ikiwa ni mwendelezo wa Afisi kutoa elimu hiyo katika Shehia mbali mbali Unguja na Pemba.*



*Kutoka kushoto, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji akiwa pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Hamza S. Johari. Kuliani ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Ndugu Shaaban R. Abdalla. Mhe. Johari alifika katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini Zanzibar kwa lengo la kuimarisha mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Afisi hizo mbili.*



*Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Ali Hamad Mbarouk akitoa elimu ya kisheria kwa wananchi wa Shehia ya Stahabu, Mkoani Pemba, ikiwa ni mwendelezo wa Afisi kutoa elimu hiyo katika Shehia mbali mbali Unguja na Pemba.*



*Picha ya pamoja ya wananchi waliohudhuria katika hafla ya kutoa elimu ya kisheria iliyotolewa na Mawakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ukumbi wa Skuli ya Bambi kusini Unguja.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji (kati kati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika halfa ya kumuaga aliyekuwa Afisa Mwandamizi Maalum Mdungi M. Mdungi (aliyevaa Koti waliokaa). Hafla hiyo ilifanyika afisini, Mazizini Zanzibar.*



*Wakili wa Serikali Mwandamizi Asya M. Ahmed akitoa maelezo kwa wananchi waliofika katika Banda la Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika maonesho Nyamanzi. Afisi imekuwa na kawaida ya kushiriki maonesho kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kazi zinazofanywa na Afisi.*




*Mwanasheria Mkuu Zanzibar Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji akimkabidhi zawadi mlezi wa Kituo cha kulea Mayatima kilichopo Mazizini mara baada ya kumaliza chakula cha Iftari kilichoandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu hapo afisini Mazizini Zanzibar.*




*Mwananchi kutoka Shehia ya Stahabu Mkoani Pemba, akichangia mada wakati Mawakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu walipofika kijijini hapo kutoa elimu ya kisheria.*



*Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Fatma Hussein Omar (kulia) akiwahudumia Wanafunzi waliofika afisini kwa uthibitishwaji wa vyeti vya kumalizia masomo kwa ajili ya kuombea Mkopo wa Elimu ya juu.*

kwa Wizara, Idara au Mtumishi wa Umma ambaye anadaiwa kutenda kosa linalohusiana na indhari hiyo.

Katika kesi ya ***Bihari Chowdhary v State (1984)2SCC 627: AIR 1984 1043:(1984) 3 SCR 309*** madhumuni hayo ya kutoa Indhari ya kuishtaki Serikali yanaelezwa vizuri. Mahkama ya juu ya India ilikuwa na haya ya Ofkusema juu ya madhumuni ya Indhari ya kuishtaki serikali:

Maudhui ya kifungu hicho ni kwamba kimetungwa kuhakikisha kuwa kabla mashtaka kufunguliwa dhidi ya Serikali au Mtumishi wa Serikali, imetolewa nafasi ya kutosha kuchuguza madai kuhusu mashtaka yaliokusudiwa kufunguliwa na kama madai hayo ni ya haki na iwapo kuna haja ya kuchukuliwa hatua za haraka ili kuepuka mashtaka yasiyokuwa na ulazima na kuokoa muda na fedha za umma kwa kuleta suluhu ya tatizo linalohusika.

Bila ya mtoa indhari kulazimika kufungua mashtaka ambayo yanaweza kumgharimu kiasi kukubwa cha fedha na muda mwingi. Serikali, tafauti na mtu binafsi inatarajiwa kuzingatia madai yaliyowasilishwa kiadilifu na baada ya kupata ushauri wa kisheria.

Kufanya uamuzi ndani ya miezi miwili kwa manufaa ya umma, kama ilivyoainishwa katika kifungu hicho kuhusu iwapo madai ya mtu anayekusudia kuishtaki Serikali ni ya haki na yana msingi, na kama madai hayo yamalizwe kwa kufanya mapatano ya haraka ya suluhu au kama yasikilizwe Mahakamani endapo kesi au shauri litafunguliwa".

Katika kesi ya ***Rizvan Dewji Popat Dhidi ya 1. Mwanasheria Mkuu, Zanzibar, 2. Ibrahim Ridha Ali; 3. Khamis Haji Ame; na Muhidin Haji Ame, Kesi ya Madai Nam. 23 ya 2022***, Mahkama iliiondoa kesi kwa sababu Mdai hakuwa ametoa notisi ya miezi miwili ya kuishtaki Serikali kama inavyotakiwa na kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Madai ya Serikali nam.3 ya 2010.

**Kufungua Shauri Mahkamani**

Baada ya muda wa miezi miwili kupita tokea kuwasilisha notisi ya kufungua madai dhidi ya Serikali, Mlalamikaji anaweza kuwasilisha madai yake Mahkamani.



***Majaji wa Mahkama Kuu Zanzibar wakiwa katika hafla ya kuapishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi Ikulu jijini Zanzibar***

Hata hivyo ieleweke kwamba Mahkama yenye uwezo kisheria kusikiliza mashauri yanayoihusu Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) na (5) cha Sheria ya Mashauri ya Madai ya Serikali 2010, ni Mahkama Kuu au Mahkama ya Mkoa.

Katika utaratibu wa usimamizi wa madai, Mwanasheria Mkuu ndiye anayetakiwa kuwa Mdaawa kwa niaba ya Serikali. Kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Mashauri ya Madai ya Serikali kinaeleza kuwa kesi yoyote ya madai baina ya Mdai na Serikali itafunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu.

Aidha, kifungu cha 10 cha Sheria hiyo kinaweka sharti kuwa Mwanasheria Mkuu au mtu mwengine aliyeidhinishwa ndiye aliyepewa uwezo kisheria kufungua kesi ya madai kwa niaba ya Serikali.

Moja ya sharti la kufungua madai mahkamani ni kulipia ada ya mahkama. Hata hivyo, kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Mashauri ya Madai ya Serikali ya Mwaka 2010 kinaeleza kuwa Serikali haitakiwi kulipa ada yoyote ya ufunguaji kesi au kupata nakla ya hukumu na amri ya mahkama.

Shufaa ambayo mahkama inaweza kutoa

Kifungu cha 12 cha Sheria ya Madai ya Serikali ya 2010 kinaeleza aina ya shufaa ambazo mahkama inaweza kutoa pale ambapo Serikali ni Mdaawa.

Kwa ujumla Mahkama inaweza kutoa amri zote ambazo inaweza kutoa katika kesi kama vile baina ya watu binafsi.

Lakini pale ambapo Serikali ni mdaawa na shufaa inayoombwa ni amri ya zuio au utekelezaji wa jambo maalum (specific performance) mahkama haitotoa amri hizo na badala yake inawezaa kutoa tamko la haki za wadaawa.

Aidha katika kesi yoyote dhidi ya Serikali ya kurejeshewa ardhi au mali nyenginezo, mahkama haitotoa amri ya kurejeshwa ardhi au mali hiyo, na badala yake inaweza kutoa tamko la kwamba mdai anastahili ardhi au mali hiyo, na kama Serikali inaihitaji ardhi au mali hiyo kwa maslahi ya taifa, taratibu za kukatisha haki hiyo zitafatwa kwa mujibu wa Katiba na sheria nyengine husika.

**Ukazaji Hukumu dhidi ya Serikali**

Mara baada ya hukumu kutolewa na mahakama, hatua inayofata ni kukaza au kutekeleza hukumu. Ukazaji hukumu hufanywa kwa kujaza fomu ya kukazia hukumu ikiambatanishwa na amri ya mahakama na hukumu husika.

Kwa kawaida, hukumu dhidi ya Mdeni Muhukumiwa inaweza kukazwa hata kwa kukamata mali yake. Kabla ya kutungwa kwa Sheria nam.3 ya 2010, hata mali ya Serikali iliweza kukamatwa na kuuzwa ili kulipa deni hilo. Sheria ya Madai ya Serikali nam.3 ya 2010, kwenye kifungu cha 16 sasa imeweka utaratibu mpya wa kukaza hukumu dhidi ya Serikali kama ifuatavyo:

Mrajis wa Mahakama baada ya kupita siku 21 tokea amri ya kulipa itolewe, anatakiwa atowe cheti chenye maelezo ya amri hiyo ya mahakama ambacho hupelekwa kwa Katibu Mkuu au Mhasibu Mkuu anayehusiana na fedha.

Katibu Mkuu atafanya malipo hayo.

Kwa vyovyote vile ni marufuku kukamata na kuuza mali ya Serikali kwa ajili ya kukaza hukumu.

Kifungu cha 17 cha sheria ya Madai ya Serikali 2010, kinafafanua mazingira ambayo Serikali imeshinda kesi na kukawa na amri ya kulipwa gharama, basi utekelezaji hukumu utafanywa kama kawaida yaani kwa kukamata mali ya Mdeni muhukumiwa na kuuzwa.

Kuhusiana na swala la utoaji hati (discovery) na udadisi wa maswali (interrogatories), kifungu cha 18 kimeweka utaratibu pale ambapo Serikali ni Mdaawa, Mahakama inaweza kuitaka Serikali kutoa hati kwa ukaguzi.

Aidha serikali inaweza kutakiwa na mahkama kujibu maswali (interrogatories). Hata hivyo uwezo huu wa mahkama hautokuwepo iwapo kufanya hivyo ni kinyume na sheria au kanuni yoyote ambayo inazuia kukaguliwa hati hizo au kujibiwa maswali ambayo ni hatari kwa maslahi ya taifa.

**Hitimisho**

Kwa kumalizia ningeweza kusema kwamba katika kesi za madai Serikali inaweza kumshtaki mtu binafsi bila ya kutoa notisi ya maandishi kwa mhusika lakini mtu binafsi hawezi kuishtaki Serikali bila ya kutoa notisi ya maandishi ya miezi miwili.

Aidha, kesi dhidi ya Serikali zinafunguliwa ama katika Mahkama Kuu au Mahkama ya Mkoa inategemea na thamani ya mali inayobishaniwa. Mtu binafsi hawezi kufungua kesi dhidi ya Serikali katika Mahkama ya Ardhi ijapokuwa kesi yake inahusika na madai ya ardhi.

Hivyo Mahkama ya Ardhi inaweza kuondoa shauri la madai dhidi ya Serikali kwa sababu haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo. Kwa mujibu wa Sheria mali ya Serikali haiwezi kukamatwa na kuuzwa kwa ajili ya kukazia hukumu iliyotolewa na Mahkama kwa ajili ya deni la mtu binafsi.

**Na Ali Ali Hassan, Mkurugenzi - wa Idara ya Usimamizi wa Kesi za Madai kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar**

# Tume ya Kurekebisha Sheria yaunganishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu

**NA MWANDISHI WETU**

**SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeiunganisha iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ili kuwa na taasisi moja itakayoleta ufanisi wa kiutendaji.**

Kwa mujibu wa agizo la Serikali, uunganishwaji wa taasisi hiyo umezingatia hali ya kiuchumi, manufaa kwa jamii, ufanisi, ubora wa taasisi ya umma, ukubwa na uwezo wa kuwafikia wananchi katika kutoa huduma.

"Katika kuzingatia hali ya kiuchumi, sera ya kuleta mageuzi na kuchochea ufanisi, Serikali imeiunganisha Tume ya Kurekebisha




***Jengo la Ofisi iliyokua Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo sasa imeunganishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar***



***Waliokua watendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria ambao kwa sasa ni Mawakili wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, wakiwa katika moja ya majukumu yao wakitoa elimu kwa Wananchi.***

Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuwa taasisi hizo zinafanana kimajukumu", agizo la Serikali lilifafanua.

Kwa mujibu wa agizo la Baraza la Mapinduzi, majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Tume hiyo, yatakuwa ni miongoni mwa majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu baada ya kuunganishwa rasmi.

Serikali imeziunganisha taasisi hizo kwa kuzingatia sehemu ya Nne ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya 2011 kuanzia kifungu cha 50 hadi 55, kinachozungumzia uanzishwaji wa taasisi katika Utumishi wa Umma na kumpa uwezo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ama kwa kushauriwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma au Mtu mwengine au Mamlaka yoyote kuanzisha, kufuta, kuunganisha au kuunda upya taasisi za umma.

Kabla ya kuunganishwa, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nambari 16 ya Mwaka 1986.

Pamoja na mambo mengine Tume hiyo, ilikuwa na jukumu la msingi la kufanya utafiti kwa kuzipitia sheria na kupendekeza marekebisho ya sheria hizo.

Aidha Tume hiyo pamoja na mambo mengine ilikuwa inafanya kazi chini ya Mwenyekiti na Makamishna ambao wote wanateuliwa na Rais, pia Tume ilikuwa na Katibu ambae pia anateuliwa na Rais.

Hivyo, ili amri ya kuunganisha taasisi hizo kufanya kazi hakuna budi Afisi ya Mwanasheria kufanya marekebisho katika Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nambari 6 ya 2013 kwa kuhuisha majukumu ya Tume na kuwa majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Hivyo Serikali ilipeleka Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali ya 2024 pamoja na mambo mengine Mswada huo ulifanya marekebisho katika kifungu cha 3 na 14 pamoja na kuweka vifungu vipya vya 23A, 23B na 31A kwa lengo la kuipa mamlaka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutekeleza kazi za Tume ya Kurekebisha Sheria.

Baada ya Mswada huo kupitishwa Baraza la Wawakilishi na kuwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali Nambari 5 ya 2024 ambayo inasomeka sambamba na Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) nambari 6 ya 2013, imefuta Sheria ya Tume na majukumu yaliyokuwa yanafanywa na Tume na sasa majukumu hayo yanafanywa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.

# Wananchi waiomba Afisi ya AG itoe elimu kupunguza migogoro ya ardhi



*Ndg. Shariff Mwalim kutoka Nungwi akitoa maoni yake kuhusu mada zilizowasilishwa wakati Mawakili wa Serikali kutoka kwa Mwanasheria Mkuu walipofika Nungwi kutoa elimua ya kisheria*

**NA MWANDISHI WETU**

**WANANCHI wa Nungwi wameiomba Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, kuendelea kutoa elimu kuhusu Sheria ya Ardhi ambayo ni muhimu zaidi kutokana na maeneo yao kukumbwa na migogoro.**

Wamesema katika Shehia hiyo, kuna ongezeko la migogoro kutokana na ongezeko la thamani ya ardhi, hivyo watakapopata elimu itawasaidia kuepukana na migogoro hiyo.

Wananchi hao walitoa ombi hilo wakati Mawakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, walipofika Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja kutoa elimu kuhusu "Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2018" na "Sheria ya Masuala ya Wazee Nam. 2 ya mwaka 2020" ikiwa ni mwendelezo wa Afisi hiyo kutoa elimu katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Mmoja ya wananchi hao, Mzee Ali Shamte alisema pamoja na jamii kukabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji msaada wa elimu ya kisheria, suala la migogoro ya ardhi limekuwa kero kubwa linalohitaji msaada wa dharura.

"Tunaishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea elimu muhimu, lakini tunaomba iandae mkutano mwengine kwa ajili ya kuelezea zaidi kuhusu masuala ya ardhi, hili ni muhimu zaidi" alisema Shamte.

Kwa upande wake Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Dkt. Abdulnasir Hikmani akizungumza na wananchi huko Shehia ya Jendele Mkoa wa Kusini Unguja, aliwashauri kulipa umuhimu suala la kusajili ndoa na



***Bw. Masoud Khamis Hamad kutoka Shehia ya Tumbe Magharibi Wilaya ya Micheweni akichangia mada wakati Mawakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu walipofika kutoa elimu kuhusu Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Sheria ya Masuala ya Wazee***

talaka kwani kufanya hivyo ni takwa la kisheria.

Aidha aliwaomba wananchi ambao bado hawajajisajili kupata vyeti vya kuzaliwa, vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi pamoja na Vifo, kuhakikisha wanalipa kipao mbele swala hilo kwani nyaraka hizo ni muhimu na zimewekwa kwa mujibu wa sheria.

Akielezea umuhimu wa kusajili nyaraka hizo, Wakili Mbarouk Mselem, alisema ni pamoja na kusaidia katika kupata fursa za kumiliki ardhi, kutafutia ajira, kupiga kura pamoja na kusafiria.

"Kwa mfano mtu anapotaka kumiliki ardhi Zanzibar lazima awe na kitambulisho cha uzanzibari, anaposafiri au kutaka kupiga kura lazima awe na vitambulisho, hivyo ni muhimu kwa ambao bado hawajajiandikisha kuhakikisha wanafanya hivyo" alisema Wakili Mbarouk.

Mdhamini wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu upande wa Pemba Ndg. Masoud Mohamed alisema lengo la kutoa elimu ya kisheria katika kijiji cha Rahakesho, Tumbe, Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuongeza ufahamu wa masuala ya sheria kwa jamii.

Awali, Dkt. Mahfoudha Ali, Wakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu aliwahimiza wananchi waliopatiwa elimu hiyo, kuipeleka taaluma jamii ili kuiwezesha sehemu kubwa ya wananchi kuwa ufahamu wa masuala ya sheria.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilifanya mikutano ya kutoa elimu kuhusu Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2018 na Sheria ya Masuala ya Wazee Nam. 2 ya mwaka 2020 katika Shehia ya Kiungani Nungwi, Bambi na Mzuri Makunduchi na kwa upande wa Pemba mikutano ilifanyika katika Shehia ya Stahabu Wilaya ya Mkoani na Kijiji cha Raha kesho Shehia ya Tumbe, Wilaya ya Micheweni.

# Mwanasheria Mkuu ampa ushauri Mkurugenzi ZMA

## Ampongeza Ndg. Mdungi kwa utumishi uliotukuka



*MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji akimkabidhi cheti cha shukran Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) Ndugu Mtumwa Said Sandali ambaye kabla ya uteuzi alikuwa mfanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar. Kushoto ni Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndugu Shaaban Ramadhan Abdalla na kulia ni Mkurugenzi Idara ya Rasilimali Watu Utawala na Mipango kutoka Afisi hiyo Ndugu Fatma Idd Ally.*

**NA MWANDISHI WTU**

**AFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, iliandaa hafla ya kuwaaga waliokuwa wafanyakazi wa Afisi hiyo baada ya mmoja kupata uteuzi wa Rais na mwengine kustaafu utumishi wa umma.**

Walioagwa ni Ndugu Mtumwa Said Sandali ambaye ameteuliwa na Rais kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) na Ndugu Mdungi Makame Mdungi aliyestaafu utumishi wa umma.

Akizungumza kwa nyakati tofauti katika hafla za kuwaaga wafanyakazi hao, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji, alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Mtumwa Said Sandali kuwa tayari kuwasikiliza wananchi watakaokuja ofisini kwake muda wote, bila ya kuwapangia siku maalum ya kufika ofisini kwake.

Mwanasheria Mkuu alisema, shida za wananchi zinaweza kutokea muda wowote hivyo ni vyema Mkurugenzi huyo kutokuwa kikwazo kufikika pale wananchi wanapokuwa na changamoto, kuwa tayari kuwasikili za kuzitatua changamoto zao.

"Mhe. Rais wetu amekuamini, hivyo jipange kufikika kirahisi kwa muda wote, hakuna haja ya kupanga siku maalum za kuonekana. Shida za wananchi zinaweza kutokea muda wowote, hivyo wanapokuja wasikilize", Dkt. Mwinyi alimsihi Mkurugenzi huyo.

Aidha amemtaka Mkurugenzi huyo kuwaunganisha wafanyakazi wa Mamlaka hiyo kuwa kitu kimoja huku akimsisitiza kusimamia maslahi yao.

Dkt. Mwinyi alimtaka kuwa na hekima na busara katika kukabiliana na migogoro hiyo na ile inayohitaji maamuzi magumu awe shupavu kufanya maamuzi hayo.

Dkt. Mwinyi alisema anafurahia

wafanyakazi kutoka taasisi yake wanapata uteuzi kwenda kutumikia maeneo mengine akiamini kuwa watakuwa na mchango mkubwa kwa taasisi hizo na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA), Ndugu Mtumwa Said Sandali wakati akitoa shukran aliwasihi wafanyakazi wa Afisi hiyo kufanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu na kwamba kila wanalolifanya wakusudie kufikia malengo ya taasisi husika.

Aidha ameushukuru uongozi na Wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ujumla wake kutokana na kila mmoja alivyochangia katika ukuaji na utendaji wake wa kazi hadi kufikia kuteuliwa katika nafasi hiyo.

Awali Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla alimuahidi Mkurugenzi Mkuu wa ZMA kila aina ya ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake ili kutimiza malengo ya Mhe. Rais pamoja na malengo ya ZMA.

Amesema Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar muda wote ipo wazi, na pale atakapohitaji msaada, Afisi itaendelea kumuunga mkono kwa faida ya Taasisi yake na wananchi kwa ujumla.

Katika hatua nyengine, kwenye hafla ya kumuaga Ndg. Mdungi Makame Mdungi, Dkt. Mwinyi alimpongeza kwa namna alivyomaliza vyema muda wake wa utumishi wa umma bila kuwa na migogoro na wafanyakazi wenziwe.

Aidha, alimsifia mtumishi huyo mstaafu kwa bidii ya kazi katika kipindi chote cha utumishi wake na hivyo kutoa wito kwa wafanyakazi wengine kuiga tabia njema za Mfanyakazi huyo.

"Sote tumejumuika hapa kumuaga Ndg. Mdungi kwa sababu ya utumishi uliotukuka, amekuwa mfanyakazi mwenye bidii na heshima kwa watu wote tena muda wote", alisema Dkt. Mwinyi.

Sambamba na hilo Mwanasheria Mkuu aliwapongeza wafanyakazi wake kwa ujumla kwa kazi wanazozifanya jambo ambalo limekuwa likiiletea sifa Afisi yake.

"Nataka nikwambieni kuwa nimekuwa nikipokea pongezi nyingi kutokana na michango yenu na ushiriki wenu kwenye Taasisi mnazoalikwa, mmekuwa msaada mkubwa kwa Taasisi hizo na kiujumla nyinyi ni watu wa thamani sana", alisema.

Kuhusu Ndg. Mdungi Naibu Mwanasheria Mkuu aliesema licha ya kustaafu utumishi wa umma bado anayo fursa ya kutoa ushauri kuhusu maendeleo ya Afisi hiyo na kwamba viongozi wanaweza kuufanyia kazi ushauri huo kwa faida ya Taasisi hiyo.




***Mstaafu Afisa Mwandamizi Maalum Ndg. Mdungi M. Mdungi akikabidhiwa zawadi ya Jokofu (fridge) pamoja na jiko la umeme na Mwanasheria Mkuu Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji.***



# “HAKI NA WAJIBU”

# Kibonzo..



NINA KESI NGUMU MAHAKAMANI NATAFUTA MWANASHERIA MZURI ANISAIDIE.
KUWA MAKINI SIKU HIZI KUNA MWANA SHERIA NA MONEY SHERIA

# Nasaha za Mshairi

## SHAIRI: UCHUMI WA BULUU NA HAMAD ALI KOMBO (DKT. MSHIKO)

**1**
Maana yake halisi Naitoa hadharani
Ili iwe ni rahisi Kuifahamu jamani
Uwatoke ukakasi Ijae mwetu vitwani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**2**
Myaka rudi myaka nenda Haukuwepo uchumi
Leo sasa umetanda Uchumi wa baharini
Vimeanzishwa viwanda Vyakuuchakata mwani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**3**
Kila kona ukienda Kusi na kaskazkni
Mezidi refu ya nyanda Wavuvi wapo kazini
Kwa boti kubwa si ngwanda Wavulia baharini
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**4**
Faiba utazipenda Zilo Tumbatu gatini
Mbio mwendo zinaenda Dakika kumi na thani
Juhudi za wetu nyonda Raisi Baba Huseni
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**5**
Wakulima wanadunda Kilimo cha baharini
Wanawakausha ng'nda Dagaa samaki ndani
Ufugaji umewanda Wa samaki baharini
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**6**
Wavuvi nao wasema Mambo sasa ahuweni
Bahari hindi nzima Waitataga majini
Samaki wakubwa jama Wawavua mkondoni
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**7**
Zile njia za kisasa Nzuri sana jamani
Ndio zimewekwa hasa Za kuvua Baharini
Ili ituze halisa Asiliye ya zamani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**8**
Pato limeongezeka Lile la serikalini
Watalii wanafika Asubuhi na jioni
Waja wakipumzika Nakuinjoi fukweni
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**9**
Na vijana kadhalika Wamengia ajirani
Kipato wanakishika Kupitia baharini
Mama wamejiegeka Kwenye kilimo cha mwani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**10**
Vizuri ikitumika Bahari nawambieni
Watalii huvutika Nawaekezaji kwani
Twapata kunufaika Dola zakimarekani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**11**
Ofisi mwanasheria Nayo imejidhatiti
Ushauri huutoa Mikataba madhubuti
Isije ngia udhia Zikaja kufujwa noti
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa Buluu

**12**
Twaona kila hatua Uchumi wenda salama
Ofisi mwanasheria Jicho latupia vyema
Hapana chenye udhia Wala kinachohasama
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**13**
Hongera naitamka Yende kwa Baba Huseni
Zanziba twatajika Kwa hili tutambuweni
Akuzidishe Rabuka Mawazo yenye thamani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

**14**
Kadi tamati nafika Nafikia kituoni
Ilahi mola Rabuka Twakuomba yamanani
Jaalia muhibaka Zanziba ya Amani
Faida zimesheheni Kwa uchumi wa buluu

# Attorney General's Chambers



AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

**Fuatilia kurasa zetu za mitandaoya kijamii.**

Afisi_ya_mwanasheriamkuu_znz

SCAN ME